USHIRIKA WA WAKULIMA WADOGO WADOGO
KILIMO CHA UMWAGILIAJI MPUNGA DAKAWA LTD
(UWAWAKUDA) S.L.P. 849, DAKAWA - MOROGORO

Kumb. Na. USHR/UWA/AJIRA/01/2024.

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

UWAWAKUDA Ltd ni Chama cha Msingi cha Ushirika wa Wakulima Wadogo wadogo Kilimo cha Umwagiliaji mpunga Dakawa kilichosajiliwa mwaka 2008 na kupewa Hati ya usajili Na. PRI-MGR-MVM-DC-2023-3850. Chama kinapatikana Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Mvomero. Chama kinajishughulisha na Kilimo cha Umwagiliaji Mpunga kwenye eneo la hekta 2000 lenye miundombinu ya umwagiliaji.

Bodi ya Uongozi wa Chama inakaribisha maombi ya kazi kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi tatu (3) kama zilivyoainishwa katika tangazo hili;-

## 1.0 MKAGUZI WA NDANI (INTERNAL AUDITOR) – NAFASI 1

**MAJUKUMU YA KAZI**

i. Kufanya mapitio ya mara kwa mara ya kumbukumbu zote za chama.
ii. Kutoa mapendekezo ya kuboresha sera, taratibu za uendeshaji na kuwasilisha kwenye vikao vya Bodi.
iii. Kuhakikisha kwamba Chama kina udhibiti wa ndani ulio imara na mathubuti kwa maslahi ya Chama.
iv. Kupendekeza kwa Bodi Wakaguzi wa nje watakaofanya Ukaguzi wa Chama.
v. Kuhakikisha kwamba vitabu vya hesabu vinafungwa kwa wakati, kumbukumbu za uhasibu zinaendana na hali halisi na zimefanyiwa malinganisho na akaunti za Chama.
vi. Kufanya Ukaguzi wa Ndani na kutoa taarifa za Ukaguzi pamoja na ushauri kwa mambo yatakayojitokeza kwa maslahi ya Chama.
vii. Kufanya Ukaguzi wa hesabu za kila Idara.
viii. Kupitia ripoti za Ukaguzi wa nje kabla ya kuwasilishwa kwenye Vikao vya Bodi.
ix. Kusahihisha na kuidhinisha hoja za Ukaguzi wa ndani;
x. Kujibu hoja za Mkaguzi wa nje zitakazojitokeza kwenye taarifa ya ukaguzi, na
xi. Kuhakikisha kuwa ripoti za ukaguzi zinaandaliwa kwa wakati na kufuatilia utekelezaji wake.

**SIFA ZA MWOMBAJI**

i. Awe na stashahada/shahada ya uhasibu kutoka Chuo kikuu kinachotambuliwa na Serikali; mwenye shahada atapewa kipaumbele cha ajira na;
ii. Awe na umri wa miaka 23 na kuendelea.

**KIWANGO CHA MSHAHARA**

- Kwa kuzingatia Bajeti ya Chama ya Mwaka 2024

## 2.0 MWENDESHA PAMPU MKUU (CHIEF PUMP OPERATOR) - NAFASI 1

**MAJUKUMU YA KAZI.**

i. Kusimamia na kuwapa maelekezo Watendaji waliopo chini yake kutekeleza majukumu yao vyema.
ii. Kuandaa bajeti ya eneo lake la kazi na kuziwasilisha kwa Meneja Mkuu.
iii. Kuandaa mpango kazi wa matengenezo na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa Meneja Mkuu.
iv. Kufanya matengenezo kama mpango kazi wa msimu unavyoelekeza.
v. Kufanya ukaguzi wa pampu kila siku.
vi. Kuendesha mitambo ya pampu na kusimamia ufanyaji kazi kwa watendaji waliopo chini yake.
vii. Kutunza kumbukumbu, kuandaa ripoti za msimu na uendeshaji wa pampu na kuwasilisha kwa Meneja Mkuu.
viii. Kuhakikisha miundombinu ya kituo cha kusukuma maji inakuwa endelevu Kutekeleza majukumu yote atakayopewa na kiongozi wake wa kazi.

**SIFA ZA MWAOMBAJI**

i. Awe na astashahada au stashahada au shahada ya ufundi wa mitambo inayotolewa na Chuo kinachotambuliwa na Serikali;
ii. Awe na ujuzi katika fani ya Fitter mechanics) daraja la tatu au zaidi.
iii. Awe na umri wa miaka 23 na kuendelea

**KIWANGO CHA MSHAHARA**

- Kwa kuzingatia Bajeti ya Chama ya Mwaka 2024

## 3.0 DEREVA (DRIVER) - NAFASI 1

**MAJUKUMU YA KAZI.**

i. Kuwaendesha Viongozi wa Chama na Watendaji/Wafanyakazi wa Chama wanapokwenda kutekeleza majukumu ya Chama nje ya Ofisi.
ii. Kuhakikisha gari na vyombo vyake vipo katika hali nzuri wakati wote na kufanya uchunguzi ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo.
iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
iv. Kutunza na kuandika daftrai la safari 'Log Book' kwa safari zote.
v. Kutunza daftari la matengenezo ya gari na kumbukumbu za vifaa vilivyofanyiwa matengenezo au vilivyobadilishwa.
vi. Kuhakikisha kwamba gari linakuwa katika hali ya usafi muda wote.
vii. Kuendesha gari kwa kufuata sheria na alama za usalama barabarani.
viii. Kutoa taarifa ya kuharibika kwa gari kwenye Uongozi ili ifanyiwe matengenezo.
ix. Kufanya shughuli nyingine atakazopangiwa na Mwajiri wake au Wakuu wake wa kazi.

**SIFA ZA MWOMBAJI**

i. Awe na Astashahada au Stashahada ya Udereva inayotolewa na Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
ii. Awe na Leseni Class C na D.
iii. Awe na umri wa miaka 23 na kuendelea.

**KIWANGO CHA MSHAHARA**

- Kwa kuzingatia Bajeti ya Chama ya Mwaka 2024

**MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI KWA KAZI ZOTE.**

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri kuanzia miaka 23 hadi 45.
ii. Waombaji wote waambatanishe vyeti vya kuzaliwa na NIDA.
iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
iv. Barua za maombi ziandikwe kwa mkono na maombi yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili na yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika na yatumwe kwa njia ya barua pepe (E-mail) uwawakuda@gmail.com yakiwa katika faili moja aina ya PDF.
v. Testimonials" Provisional Results" Statement of results" hati za matokeo za kidato cha nne na sita havitakubaliwa.
vi. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
vii. Waombaji watakaokidhi vigezo ndiyo watakaoitwa kwa ajili ya usaili.
viii. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 29 Februari, 2024 saa 10:00 jioni.

Muhimu, kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu. Anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa:-

**MWENYEKITI WA BODI,**
**UWAWAKUDA LTD,**
**S.L.P 849,**
**MOROGORO.**

**Imetolewa na;**

**Joseph E. Lutango**
**MWENYEKITI WA BODI**

TCL Epaper Copy